

Tamko na Sala ya Kukana kujikweza

Nakushukuru Baba kwa kuwa nimeumbwa kwa jinsi ya ajabu, Kwa sababu wewe ndiwe uliyeniumba. Asante kwa sababu wewe unanipenda na unaniita kuwa ni wako mwenyewe. Asante kwa kunipa nafasi ya kumfuata Yesu Kristo.

Nakusihhi tafadhali unisamehe kwa kuendeleza tabia ya kujiona kuwa bora kuliko wengine. Nakana na nakataa kabisa tabia za namna hiyo. Nakataa hali ya kujisikia vizuri kuwa bora zaidi ya wengine. Ninakiri kuwa mimi ni mwenye dhambi, kama watu wengine wote, na siwezi kufanya lolote bila wewe.

Vilevile ninatubu na kuzikana hisia za kujiona mimi ninatoka katika kundi lililo bora zaidi au lenye makuzi bora zaidi. Ninatambua kuwa watu wote ni sawa mbele zako.

Ninatubu kwa kutamka maneno ya dharau kwa wengine na kuwakataa wengine, na ninaomba unisamehe kwa maneno yote hayo.

Nakataa kuwawazia wengine kuwa hawafai kitu kwa sababu ya rangi yao, jinsia yao, utajiri wao, au elimu yao.

Ninatambua kuwa ni kwa neema ya Mungu tu kuwa ninaweza kusimama mbele zako. Ninajitenganisha na hukumu zote za wanadamu, na ninakuangalia wewe tu upate kuniokoa.

Kwa umahsusi kabisa nayakataa mafundisho ya Kiislamu kuwa watu wenye haki ndiwo walio bora zaidi, kuwa Uislamu unawafanya wawe na mafanikio, na kuwa Waislamu ni bora zaidi ya wasio Waislamu.

Nakataa na kuyakana madai kwamba wanaume ni bora zaidi ya wanawake.

Baba wa mbinguni, ninageuka mbali na kila hisia bandia ya kujiona kuwa bora na badala yake nachagua kukutumikia wewe.

Bwana vilevile nachagua kufurahia mafanikio ya wengine. Nakataa na kukana aina zote za kijicho na wivu kwa watu wengine.

Bwana nakusihhi unipe uamuzi mzuri na sahihi unaohusu vile nilivyo ndani yako. Nifundishe ukweli wa vile unavyoniona mimi. Nisaidie niweze kuridhika kama mtu yule uliyemuumba awe.

Amina.